# Huu Ni Wakati Wa Bibi Arusi

*Ufunuo:3:20*

*Tazama nasimama mlangoni,nabisha;(Kristo*
*Akiwa nje ya kanisa-Neno limefungiwa nje kwa ajili*
*Ya taratibu za kidhehebu!)..mtu akiisikia sauti yangu,*
*Na kufungua mlango,nitaingia kwake,*
*Nami nitakula pamoja naye,na yeye pamoja nami*.

Sikiliza kile ambacho nabii wa Mungu amesema katika wakati huu wa mwisho:

Tuko katika siku za mwisho.Sisi sote tunajua hilo.Na tuko tayari kwa ajili ya kuja kwa Bwana.Jambo la kufanya ni kujitenga na kila dhambi.Jitenge na kitu chochote kinachofanana na ulimwengu/dunia.Usiipende dunia wala mambo ya dunia.Usiache mtu yoyote,kwa kanuni zake,akudanganye.Kaa kwa usahihi kabisa katika ahadi za Mungu,Neno la Mungu; na hilo Neno,kama ni Neno, la siku ya leo, Mungu analithibitisha hivyo.Kama hafanyi hivyo,basi sio Neno la siku ya leo,Neno lililokuja siku ya Pentekoste halitafanya kazi katika siku hii ya leo.Hapana,Bwana.Hilo lilikuwa kwa wakati wa Pentekoste.Hili ni kwa ajili ya Bibi Arusi;Kwenda nyumbani kwa Bibi arusi.Tunacho kitu tofauti.wapentekoste waliwakilisha hao.Tuko wakati wa Bibi Arusi.Kama vile Neno la wakati wa Noa lisingeweza kufanya kazi katika siku za Musa isingeweza kufanya kazi katika siku za Paulo.Yeye hapa anajaribu kuwaambia hao kwamba“Mmekufa kwa hiyo.(torati)Na hamuwezi kuitegemea/kuwanayo”(Wagalatia 3:21-28; 2:19-21).

Kanisa,ninyi ambao ninazungumza nanyi usiku huu wa leo nchini kote.Kama umejitenga mwenyewe kutoka katika madhehebu na uchafu wote na mambo ya dunia hii, na vitu vyote ambavyo vina kuweka wewe katika kanuni zilizoundwa na watu na taratibu na vitu kama hivyo umejitenga mwenyewe, angalia juu. Kuwa tayari.Ule moto utaenda kushuka moja ya siku hizi.Mungu ataenda kumuachia aje,katika sura ya kuvutia.Utakuwa tayari akija? kule kunyakuliwa kwa Bibi arusi wa namna ya kimbinguni….Atakuwa ameumbwa kutoka afaye kuwa asiye kufa;ageuzwe mara moja katika kufumba na kufumbua jicho(1Kor15:51-54) sisi tulio hai tutakaobakia hatutawatangulia wale waliokwisha kulala (1Wathesal 4:13-18) [1]

Je Yesu hakunena juu ya siku za mwisho (Mathayo 24:24) zile Roho mbili zitakuwa karibu sana kiasi cha kudanganya zile chembe, zilizojulikana kimbele, wale walioteuliwa kama ingewezekana karibu sana/inafanana na kitu halisi,ndivyo ilivyo siku za mwisho…….Sasa, unaona, ni wakati wa ngano sasa, Tunafikia wakati wa mavuno. Huu siyo wakati wa Luther; huu siyo wakati wa Pentekoste; huu ni wakati wa Bibi arisi.

Kama vile Musa alivyotoa taifa ndani ya taifa (Kutoka 3:1-10). Kristo leo anaita kanisa kutoka ndani ya kanisa (unaona?) Jambo lile lile kwa mfano/kulinganisha, kuwachukua wao kwenye nchi ya ahadi, utukufu wa milele.

Sasa, kumkataa yule mtu aitaye, Kristo, haijalishi kwamba wewe ni Mpentekoste, Mmethodist, Lutheran ,chochote uwacho,ni lazima uwe na…….sina chochote kinyume nao. Sina hata kidogo lakini katika wakati huu inabidi kama walivyofanya katika wakati ule utu wa Yesu Kristo ambao ni Neno.Hapo mwanzo kulikuwako Neno.Naye Neno alikuwa kwa Mungu. Naye Neno alikuwa ni Mungu.na Neno akafanyika mwili.Naye akakaa kwetu, Ni yule yule jana leo na hata milele Yohana1:1-5,14,(Waebrania 13:8) unaona? Lazima umkubali huyo mtu wa uzima wa milele(Yohana1:12-13).

Sasa, uhai aliokuwa nao Luther, ni kuhesabiwa haki kwa imani.Wesley alikuwa na utakaso ulio-ongezwa katika huo. Pentekoste alikuwa na kurudishiwa vipawa vikiturudia na kuongezwa katika huo .Lakini sasa ni kukamilishwa katika mwili(unaona?),Zile hatua tatu za hilo na kutokana na huyo……Halafu saa ufufuo unakuja,uhai ulioishi ndani ya Waluteri huo ulitoka nje.Uhai ulioishi ndani ya wamethodist na ukatoka.Uhai ulioingia ndani ya Wapentekoste, wote huo utanyakuliwa kutoka mavumbini Katika Mwili wa Bibi Arusi na kuchukuliwa mbele za Yesu Kristo (Wathes 4:16-17),utukufu kwa Mungu.oh inasisimua, huo ni ukweli.

Tumepiga kona, tunaangalia kuelekea mbinguni (Luka 21:28).Tukiangalia kule kuja kwa kifuniko juu ya pyramid,kama ambavyo tungesema, kule kurudi kwake tena.Kanisa lazima litafufuliwa karibuni,na ni lazima tuwe tayari(Ufunuo 20:5-6) [2]

Sisi hatuishi katika wakati wa Pentekoste:tunaishi katika wakati mwingine.Unaona?hatuishi katika wakati wa Methodist tunaishi katika wakati mwingine.Tunaishi hapa juu katika wakati wa Bibi Arusi, kule kuingia na kutoka kwa kanisa na kukusanyika pamoja kwa ajili ya unyakuo.Huo ndio wakati tunaoishi sasa.Kwa ukamilifu wa maoni yangu hiyo ni kweli kabisa.Na unaweza ukawa mwaminifu sana;lakini mpaka tujue kile tunachokifanya unapigana na hewa.Kama askari hajui cha kufanya mpaka apokee amri ya kutenda tunatakiwa tuwe

askari wa kikristo na kupata maagio/amri kutoka kwenye Biblia kwa ajili ya saa hii;sio agizo la jana,agizo la siku kabla ya jana,lakini agizo la leo jinsi tupaswavyo kwenda.Tutafute tujue saa tunayoishi.Matendo 3:19-21),Luka17:26-36; 2Wathes 2:1-3; 2Tim 3:1-5).

Na matukio haya ya kisasa yanatupita kwa haraka,na siku moja tutakuja kuona kwamba tumeachwa nyuma bila kitu,na tunapaswa kutiwa muhuri kwa chapa ya mnyama.kabla hatujalifahamu hilo(Ufunuo. 13:16-18).

Sasa,na subira inabidi tungojee hili, kwa unabii ule ulioahidiwa,kila mmoja inabidi utimizwe katika wakati wake(Waefeso 5:25-27;Ufunuo 10:8-11).Kwa maana inatuambia kimbele.Yule mwanzilishi alilitenda hili kabla,na tunasubiri tumwone yeye akilifanya tena.Ni wakati wa ajabu tunaoishi, na unaangalia Biblia ya Mungu kujua ni wakati gani unaoishi(Ufunuo 3:14-21)

Hatuishi katika wakati wa Wamethodist, wakati wa Baptist.Tunaishi katika wakati wa Bibi Arusi,wakati wa kuitwa,kurudishwa tena kwa Mungu kupitia njia Yeye aliyoiahidi,ili kuturudishia,aliahidi kufanya hivyo(Ufunuo 10:7;Malaki 4:5-6,[3:23-24] Matayo 17:11). [3]

Sasa,inaanza kujitenga, Ngano inaanza kuonekana huu wakati wa Kipentekoste; huu ni wakati wa baadaye, wakati wa Bibi Arusi,hii ni nuru ya wakati wa jioni(Zakaria 14:6-7) ni wakati malaki 4 inapotimizwa fuata mkanda.

Huu ni upendo hili ni Luka 17:30 ikitimizwa;hiki nikitabu cha Yeremia oh na vyote vilivyobakia. Kwamba Yoeli alizungumza juu ya siku hizi Yoeli2:28-32.Hii ndio siku ile.Nimesikia,Bwana,kwamba inakuja,lakini sasa naliona kwa macho yangu"(ayubu 42:1-6) [4]

Angalia,kuishi katika kivuli cha luther,kuishi katika kivuli cha Wesley,kuishi katika vivuli nyuma pale.Hiyo ndiyo sababu hayawezi kuona nuru ya kweli. Kama wangesimama kwa dakika chache tu na kushika Biblia na kuisoma hiyo,wangeona kwamba hii ni nuru iliyo ahidiwa kwa saa hii(Yoh.12:35-36)

Sasa,tutaenda kuchukuwa baadhi ya vitu hivi kwa dakika.Aliahidi kulingana na Malaki 4:5-6 mambo haya yangetokea.ameahidi yote kupitia maandiko yote kwamba yangetokea.Angalia Israel pia,mfano wetu,katika safari(Angalia).Kuna namna ambayo ilikuwa uhai wao,ambayo iliwapa nguvu,uhai,hiyo nisawa? Israel hawakuweza kula manna ambayo ni ya iliyoanguka jana.(Kutoka16).ilikuwa ina wadudu;ilikuwa imeoza;haikuwa nzuri kwa ajili yao;wangewauwa.Ile manna iliyo wafanya waishi jana itauwa leo.Biblia ilisema ilikuwa na wadudu ndani yake,iliharibika.Walipaswa kupata manna mpya kila siku.Amen.Nani nini? Watu wanaishi kwa manna ya Luther,Wesley,na wote kule nyuma, mnakula chakula kilicho na wadudu ambacho kitawauwa kiroho.Unaona? Kinawauwa ninyi mfe katika kanuni zenu

Manna ya jana, ya Luther isingefaa kwa wamethodist manna ya Wamethodist haitafaa kitu kwa Wapentekoste.Manna ya Wapentekoste haitaweza kutufaaa leo.Unaona ninacho maanisha kila siku inakuja siku kwa siku,iliyo safi,kadhalika ndivyo ilivyo katika nyakati saba za kanisa.Manna ya lutherani.ilikuwa ni ujumbe wa kuhesabiwa haki.ujumbe wa Wesley ulikuwa udhihirisho wa utakaso;Pentekoste ilikuwa kurudishiwa vipawa.Lakini hii inalitambulisha jiwe/kifuniko,siku za mwisho.Mti wa Bibi Arusi ni kinyume na vyote.Na bado ni nuru ile ile kwa wale waliokomaa,kama jua lile lile linaloangaza leo(Desember) je ataikomaza mbegu leo kwa ajili ya mavuno katika July.unaona kile ninacho maanisha? Lakini nuru leo( katika Desember) haitafanya vizuri nyuma pale July.bado ina nguvu.Ngano itakuwa imesogea zaidi.Na kuwa tayari kuvunwa.Amen.Hakika hiyo haiwezekani sasa baadaye inawezekana.Sababu haikuwa pale pale Ni sasa hivi. [5]

Matayo 24:28 "kwa kuwa popote ulipo mzoga, ndipo watakapo kusanyika tai."Mzoga ni nani na tai ni nani?(Luka 17:36:) Mzoga ni nini? Mzoga ni kile wanacho kula tai.Sasa,tai katika biblia inakuwa ni Nabii.Nabii ni tai.Mungu anajiita Yeye mwenyewe ni Tai (Kumbukumbu 32:11-12).na sisi ni watoto wa tai basi, waaminio.Unaona? na sasa huo mzoga ambao wanakula ni nini? Ni Neno. Popote Neno lilipo,asili ya kweli ya ndege itajidhihirisha yenyewe.Unaona? Tai, anapenda nyama ambayo ni fresh,Lazima apate nyama fresh.Yeye sio kunguru;yeye ni tai.Huwezi ukampa chakula cha kidhehebu yeye,lazima apate chakula cha tai;hiyo ndiyo nyama ya sasa hivi iliyo tengenezwa,siyo alichofanya Musa,siyo kile alichofanya mtu fulani.Siyo Sankey, Finney, Knox, Calvin, lakini sasa hivi, nyama iliyo uwawa ya siku ya leo.Na hiyo ni sehemu ya Kristo iliyo kufa kulifanya hili Neno lithibitike.Hiyo ndiyo wanayo kula.Unalipata hilo?

Siyo kile Noah amefanya,Musa alichofanya,wao ni mfano;tunasoma na kuona walivyofanya,lakini ni kile alicho ahidi kufanya sasa(Waefeso1:15-19).Alikuwa ni Neno nyuma pale;huo ulikuwa mzoga wa siku ile.Siku ya Wesley ilikuwa ni mzoga wa siku ile;siku za Luther ilikuwa ni mzoga wa siku zile; lakini hawaendi nyuma kwenye hayo.Tayari hayo yameharibika kile kilicho bakishwa ni lazima kichomwe.Hata kile cha meza ya Bwana.Usikiache kwa ajili ya kizazi kingine.Biblia inasema unaposhiriki meza ya Bwana,kile kinachobakia usikiache kilale mpaka asubuhi; kichome, kwa hiyo tukirudie hicho? Hapana, Bwana.Tuna chakula cha leo;hilo ni Neno

lililo ahidiwa la saa hii ili lidhihirishwe katika saa hii (1Yoh3:1-3;Matayo25:6).Hapo ndipo tai walipo,mahali ulipo mzoga.Tunaweza kukaa muda mrefu kwenye hilo.Lakini nina uhakika mnaelewa kile ambacho ninamaanisha. [6]

Angalia ni mawazo ya kwanza ya Neno la Mungu (Matendo 26:22-23).Na leo, kwa sababu alikuwa ni Mwana wa kwanza wa Mungu kuja katika ukombozi mkamilifu kuwa ndani ya Mungu,aliondolewa kutoka duniani na akatikiswa juu ya watu( oh ni somo tukufu jinsi gani) kwa nguvu za kuhuisha.alitikiswa juu ya mbegu ambayo iliahidiwa uzima.alitikiswa siku ya Pentekoste(Matendo 2:1-21),ilipotoka sauti kutoka mbinguni kama uvumi,wenye nguvu, upepo wa kasi na ukatikiswa juu ya watu,watu wa Pentekoste ambao walikuwapo pale pentekoste wakiingojea baraka iwajilie (Luka24:48-53); na unapaswa utikiswe tena,tunafahamu katika siku za mwisho, kutokana na (Luka17:30),ndani ya mwana tena, katika siku ambayo Mwana wa Adamu atafunuliwa au atatikiswa tena mbele ya watu na mafundisho yote ambayo tunayo na uthibitisho wa Neno la Mungu,kwa Neno la Mungu,kwa ishara,na maajabu,tunaona leo,Neno tena linatikiswa mbele ya watu.Kwamba kanuni mfu za watu zimekufa na Mwana wa Mungu anaishi tena akiwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu miongoni mwetu na anatupa uzima.kama vile Kristo alivyokuwa wa kwanza kufufuka miongoni mwa manabii wote na kadhalika,(ingawaje ametokea mfano katika sehemu mbali mbali.alikuwa matunda ya kwanza ya wale waliolala),(1Kor15:20-23;Matendo26:22-23), katika Bibi Arusi katika wakati wa kuja kwa Kristo, kutoka kwenye makanisa,kutakuwa na mganda utakaotikiswa tena katika siku za mwisho,oh jamani.

Kule kutikiswa kwa mganda,mganda ni nini? Ule wa kwanza uliokuja kukomaa (Walawi 23:9-14),ule wa kwanza ulithibitisha kuwa ilikuwa ngano ambayo ni mganda. Hallelujah. Nina uhakika unaelewa kile ninachozungumzia.ulitikiswa mbele ya watu.Na kwa mara ya kwanza pale utakuja kwa wakati wa Bibi Arusi, Kwa ufufuo kutoka kwenye giza la madhehebu,kutakuwa na ujumbe ambao ukomavu mkamilifu wa Neno utarudishwa tena katika ukamilifu wa nguvu zake na kutikiswa juu ya watu kwa ishara zile zile na majabu ambayo uliyafanya nyuma pale.

“kwa sababu ninaishi,tutaishi pia”akimzungumzia mkewe. “kwa sababu ninaishi,utaishi pia”(Yohana 14:18-20) ni ufunuo wa namna gani ulivyo kuwa.Na ni ufunuo ulioje:kuhuishwa kutoka kwa wafu, kufanywa hai ndani ya Kristo kwa nguvu ya kuhuisha ya Mungu (Waefeso 2:1-7).Alitikiswa kwao;ambaye Yeye alikuwa Neno, lilitikiswa tena kwao siku ya Pentekoste.Neno likadhihirishwa.Na kama nisemavyo,inatikiswa tena katika siku za mwisho. [7]

Nukuu za kiingereza
[1] Muungano usioonekana wa Bibi Arusi uk.46
[2] Uongozi 65-1207,Aya 140-144
[3] Matukio ya kiwekwa wazi na unabii(65-1206 Aya 56,60-62
[4] Nimesikia bali sasa naona Aya 187/
[5] Yupo mtu hapa anaye weza kuwasha taa Aya 159-162
[6] Maswali na majibu(64-0823m) kitabu cha COD swali No239
[7] kuchomoza kwa jua uk.14-16

*jiwe la kiroho la kujengea na 175. kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*